

**HOTUBA YA MHE. JUMAA H. AWESO (MB) WAZIRI WA MAJI  
KWENYE UWEKAJI WA JIWE LA MSINGI MRADI WA MAJI MJI WA  
KALIUA TAREHE 29/07/2023**

- *Dr. John R. Mboya, Katibu Tawala Mkoa (RAS) na Mwakilishi wa Mkuu wa Mkoa wa Tabora,*
- *Mheshimiwa Onesmo Selemani, Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kaliua*
- *Ndugu Eliud Shemaiya, Katibu wa CCM Wilaya ya Kaliua*
- *Mhe. Dr. Rashid M. Chuachua, Mkuu wa Wilaya ya Kaliua*
- *Ndugu Kilakala Katibu Tawala Wilaya ya Kaliua*
- *Mhe. Andrea A. Kwezi, Mbunge wa jimbo la Kaliua*
- *Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ya Kaliua*
- *Mkurugenzi wa Usambazaji Maji na Usafi wa mazingira Wizara ya Maji,*
- *Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira TABORA,*
- *Meneja RUWASA Mkoa wa Tabora*
- *Mkandarasi wa miji 28 Megha engineering Ltd*
- *Mhandisi Mshauri wa Miji 28 WAPCOS*
- *Ndugu Viongozi wa Sekta ya Maji mliopo hapa leo,*
- *Menejimenti na Watumishi wa Sekta ya Maji Mkoa wa Tabora- TUWASA, RUWASA na BONDE,*
- *Viongozi wa Dini, Wanahabari,*
- *Wananchi wa Kaliua*
- *Mabibi na Mabwana, Itifaki imezingatiwa.*

**"Nawasilimu kwa jina la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania"**

Awali ya yote, Ninapenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kuwepo katika siku hii ya leo

### **Ndugu Katibu Tawala-Mkoa wa Tabora**

Nachukua nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kuambatana nami katika ziara hii fupi ukimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tabora Mhe. Dr. Batilda Salha Burian. Naomba unifikishie salaam zangu za dhati kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa.

### **Ndugu Wananchi**

Wizara ya Maji inatambua kuwa hali ya upatikanaji wa Maji katika wilaya ya Kaliua siyo ya kuridhisha, Mahitaji ya Maji kwa sasa katika Wilaya ya Kaliua ni wastani wa lita 16,961,175 kwa siku wakati upatikanaji wa maji kwa sasa ni wastani wa lita 7,971,752 kwa siku. Kwa ujumla Wilaya ya Kaliua ina upungufu wa lita 8,989,423 kwa siku.

Kwa Mji wa Kaliua mahitaji ni lita 1,535,150 kwa siku wakati uzalishaji ni lita 675,466 hivyo kuwepo na upungufu wa lita 859,684 na kufanya Hali ya upatikanaji wa maji mjini kuwa 44%

Kwa upande wa Vijijini, mahitaji ni lita 15,426,025 kwa siku lakini maji yanayozalishwa ni lita 7,250,232 na kuwa na upungufu wa lita 8,175,793 na kufanya hali ya upatikanaji wa maji Vijijini kuwa 49%.

## **Ndugu Wananchi**

Wizara inaendelea kutekeleza miradi mbalimbali nchini ili kufikia malengo yaliyowekwa na Ilani ya CCM kwamba ifikapo 2025 Upatikanaji wa maji mijini uwe asilimia 95 na Vijijini uwe asilimia 85

Aidha, kwa Mkoa wa Tabora Miradi mbalimbali imetekelezwa na miradi mingine imepangwa kutekelezwa ikiwemo mradi wa miji 28

## **Ndugu Wananchi**

Leo nimeweka jiwe la Msingi wa Mradi wa Maji Katika Mji wa Kaliua unaogharimu **Shilingi milioni 503.1** ambao utaongeza upatikanaji wa maji kutoka 44% hadi 50% kwa wakazi wa mjini Kaliua (Watu 3,700 sawa na Kaya 617).

## **Ndugu Wananchi**

Katika mradi huu, Serikali imelipia pia sehemu ya gharama za vifaa vya kuunganisha wateja 110 watakojitokeza mapema baada ya kukamilika kwa mradi. Wateja hao watalipia shilingi 100,000/- tu ili waunganishiwe maji majumbani mwao badala ya wastani wa shilingi 300,000 hadi 400,000.

Nimefahamishwa kuwa, Wateja 14 tu ndiyo wameshalipia mpaka sasa, Hivyo nawasihi wananchi wajitokeze ili waunganishiwe maji kwa gharama nafuu.

## **Ndugu Wananchi**

Nimeona utendajikazi wa Mkandarasi na ninaelekeza mradi huu ukamilike mwezi Agosti, 2023 kama ulivyopangwa ili Wananchi wa Mji wa Kaliua wanufaike na kazi kubwa ambayo Mhe. Rais anaifanya ya kumtua mama ndoo kichwani.

Suluhu ya kudumu ya tatizo la Maji katika Wilaya ya Kaliua ni Mradi wa Miji 28 ambao kwa Mkoa wa Tabora unatekelezwa kwenye Miji ya Kaliua, Urambo na Sikonge. Serikali imetenga jumla ya Dola za Marekani Milioni 62.28, Sawa na shilingi Bilioni 143.26

Mradi huu utatoa maji ya ziwa Viktoria kutoka Tabora hadi Kaliua na utatosheleza mahitaji ya Maji kwa Miji ya Kaliua, Urambo na Sikonge hadi mwaka 2040. Tayari Wizara imeshaajiri Mkandarasi *Megha Infrastructure company limited* ambaye niko naye hapa na tumemwelekeza akamilishe mradi huu mwezi Oktoba, 2025

Kukamilika kwa mradi huo kutaboresha upatikanaji wa maji kutoka 50% hadi zaidi ya 95% kwa mji wa Kaliua.

## **Ndugu Wananchi**

Tuendeleo kushirikiana katika kuhakikisha miundombinu ya mradi huu ikiwemo vyanzo vya maji na miundombinu ya bomba vinalindwa ili huduma iwe endelevu.

Mwisho, nirudie tena kushukuru kwa kushiriki katika hafla hii ya uwekaji wa jiwe la Msingi katika mradi huu wa maji Mji wa Kaliua

## **ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**